



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

BODI YA WATAALAMU WA UNUNUZI NA UGAVI (PSPTB)



TAARIFA KWA UMMA

USAJILI WA MITIHANI YA 23 YA BODI

DAR ES SALAAM 02 AGOSTI, 2021

Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kwamba, imefungua dirisha la usajili kwajili ya mitihani ya 23 itakayofanyika nchini mwezi Novemba, 2021. Mitihani hiyo inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 23/11/2021 mpaka tarehe 26/11/2021. Watahiniwa wote wanaelekezwa kufanya usajili wao kwa njia ya mtandao kupitia <https://registration.psptb.go.tz> na kuhudhuria madarasa kama sehemu ya maandalizi ya mitihani. Mwisho wa kutuma maombi kwa ajili ya mitihani hii ni tarehe 15-10-2021.

SIFA ZA WAOMBAJI KWA AJILI MITIHANI YA NOVEMBA, 2021:

- (1) Wanafunzi wote waliomaliza vyuo vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za shahada, stahada na astahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia Julai 2021 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi.
- (2) Wanafunzi wote waliofanya mitihani ya Bodi kipindi cha nyuma na matokeo yao yalishatoka lakini bado hawajamaliza au wana masomo ya kurudia wanakaribishwa kusajili ili kuweza kufanya mitihani hii ya kitaaluma kabla ya mtaala kubadilika.
- (3) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi wasiokuwa na CPSP na wanaotaka kupata sifa hiyo pamoja na wale wote wanaohitaji kupanda katika ngazi ya usajili wa Bodi kitaaluma au kupanda madaraja ya kazini kwa mujibu wa Waraka Na. 3 wa 2015.
- (4) Watahiniwa wote wanaosubiri matokeo ya **mtihani mmoja** kati ya mitihani ya **mwezi Agosti, 2020, Novemba 2020 au Mwezi Juni, 2021** wanaruhusiwa kujisajili kwa ngazi inayofuata.

NB. Kwa wale wote ambao walifanya mitihani ya mwezi Agosti, 2020, Novemba, 2020 na Juni, 2021 kwa mfuatano na matokeo yao bado hayajatoka waendeleo kusubiri mpaka matokeo yao yatakapo tangazwa ama kuelekezwa vinginevyo.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi piga simu namba 0738441972 au tuma barua pepe kupitia examinations@psptb.go.tz

Imetolewa na

Godfred B. Mbanyi

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI

Keko Mwangi (Majengo ya Bohari), S.L.P. 5993, Dar es Salaam. Simu: +255 22 2865860
Nukushi: +255 22 2862138. Tovuti: <http://www.psptb.go.tz> Barua pepe: info@psptb.go.tz